Jarida la Kiswahili Sanifu

Ubadilishaji Msimbo katika baadhi ya Nyimbo za Ohangla

Akello Odiaga Walter
Chuo Kikuu cha Kisii; walterodiaga@gmail.com

IKISIRI

Makala hii ilichunguza aina za ubadilishaji msimbo katika baadhi ya nyimbo za Ohangla. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Maki iliyoasisiwa na Myers-Scotton (1993). Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kueleza aina za ubadilishaji msimbo zinazotumiwa katika baadhi ya nyimbo za Ohangla. Ili kufikia lengo hili, utafiti ulichunguza nyimbo nne za Ohangla zilizotungwa na Prince Indah na Vicky B. Matata. Nyimbo za wasanii hawa ziliteuliwa kutokanana na umaarufu wao miongoni mwa wapenzi wa nyimbo za Ohangla. Utafiti huu ulitumia sampuli kusudio katika kuteua wasanii hawa pamoja na nyimbo zilizochanganuliwa. Katika kukusanya data mtafiti alisikiliza na kurekodi data kutoka kwa nyimbo hizi kupitia mtandao wa Youtube. Kupitia kwa mihimili ya nadharia ya utafiti, data za utafiti zilichanganuliwa kwa kutoa maelezo. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa wasanii wa nyimbo za Ohangla hutumia aina tatu za ubadilishaji msimbo, yaani, ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi, ubadilishaji msimbo baina ya sentensi na ubadilishaji msimbo kileksia. Makala hii inahitimisha kuwa mbinu ya ubadilishaji msimbo katika nyimbo za Ohangla ina athari chanya miongoni mwa wapenzi wa nyimbo hizi kwani inawasaidia wasanii hawa kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kufidia upungufu wa msamiati katika lugha solo.

KUHUSU MAKALA

Maneno Muhimu:
Lugha solo, Ohangla, Ubadilishaji msimbo

Historia ya Makala:
Tarehe ya Kutumwa:01 Mei 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 08 Agosti 2026
Tarehe ya Kukubalika:20 Agosti 2026
Mtandaoni: 09 Oktoba 2026

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254**712058021**; *Barua Pepe* walterodiaga@gmail.com
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Akello, O.W. (2026). Ubadilishaji Msimbo katika baadhi ya Nyimbo za Kiswahili. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(2), 121-129
© 2026
Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

1. Utangulizi

Kulingana na shirika la *Ethnologue*, nchi ya Kenya ina zaidi ya lugha na lahaja 60 zinazotumiwa katika mawasiliano. Hali hii huchangia kuzuka kwa uwili na wingi lugha miongoni mwa watumizi wa lugha. Uwili lugha ni hali ya mtu kuwa na uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi kimbadilishano. Hali ya uwili lugha hutokea wazungumzaji wengi ndani ya jamii husika wana umilisi wa lugha zote mbili (Wahyuni, 2017). Kuwepo kwa uwili na wingi lugha katika jamii huchangia kuwepo kwa hali ya kubadili msimbo katika mawasiliano. Kubadili msimbo ni hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika diskosi.

Kuwepo kwa wingi lugha kunasababishwa na maingiliano baina ya jamii zinazozungumza lugha tofauti, lugha moja kuwa na hadhi na staha ya kijamii, ukuruba wa kimaeneo ambapo mzawa wa lugha huwa na nafasi kubwa ya kumiliki lugha ya eneo jirani, sababu za sera ya elimu na sababu za kiuchumi. Myers Scotton (1993) anaeleza kuwa kubadili msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo, bila kutohoa fonolojia ya lugha moja ili iingiliane na nyingine.

Kachru (1978) anadai kuwa kubadili msimbo hurejelea uhamishaji wa elementi za kiisimu kutoka lugha moja hadi nyingine. Elementi hizo zinaweza kuwa mofimu, maneno, kirai, kishazi au sentensi. Kulingana na Bokamba (1989), ubadilishaji msimbo ni hali ya kuchopeka vipengele mbalimbali vya kiisimu kama vile viambishi, maneno, na vishazi vinavyotumiwa na washiriki katika mazungumzo kuelezea mawazo ambayo washiriki wenza wanafahamu au wanaweza kufahamu.

Msimbo ni lugha au lahaja yoyote iliyoteuliwa na kutumiwa katika muktadha fulani. Aghalabu, watumizi wa lugha hubobea katika matumizi ya msimbo fulani kuliko mingine. Kulingana na Akinseye (2016), hali ya kubadili msimbo hujitokeza katika kiwango cha diskosi, sentensi au vipengele vyake. Kubadili msimbo ni tukio la kawaida la kijamii na hujitokeza katika shughuli za kijamii kama vile nyimbo.

Wataalamu mbalimbali kama vile Wanjiru (2014) na Arifin (2018) wameafikiana kwamba mbinu ya kubadili msimbo hutumiwa na wasanii kutokana na uraibu wa kutumia misamiati fulani au upungufu wa misamiati wa kueleza dhana fulani. Matumizi ya lugha mbili kwa pamoja ni hali inayoendelea kushamiri katika jamii ya Waluo hususan katika utunzi wa nyimbo. Hali hii huenda inatokana na haja ya wasanii kutaka kudhihirisha umilisi wao wa lugha ya pili, kukosa msamiati mwafaka katika lugha solo au kutaka kusisitiza jambo fulani. Ubadilishaji msimbo hautokei kiholela, bali huwa kuna lengo na umantiki katika kubadilisha lugha. Utafiti huu ulinuia kuchunguza aina za ubadilishaji msimbo katika nyimbo za *Ohangla*.

2.0 Suala la Utafiti

Ubadilishaji msimbo si jambo geni katika muziki. Watunzi wa miziki hutumia mbinu hii ili kutimiza majukumu fulani, yakiwemo kufidia upungufu wa msamiati katika lugha solo na kudhihirisha umilisi wa wingi lugha. Tafiti anuwai zimefanywa kuhusu majukumu, aina na vichocheo vya ubadilishaji msimbo katika baadhi ya lugha za Kiafrika na Kiingereza. Hata hivyo, utafiti wa aina hii unakosekana katika nyimbo za kitamaduni katika jamii ya Waluo, almaarufu *Ohangala*. Lugha ya Dholuo ambayo ndiyo lugha solo, inazidi kuingiliana na lugha nyingine kama vile Kiswahili na Kiingereza. Makala hii inaangazia aina za ubadilishaji msimbo katika nyimbo za *Ohangla*. Inachanganua ubadilishaji msimbo baina ya lugha solo ya Dholuo na Kiswahili na Kiingereza.

3.0 Mapitio ya Maandishi

Sehemu hii inaangazia yaliyoandikwa kuhusu Ohangla na Ubadilishaji Msimbo.

3.1 Yaliyoandikwa kuhusu Ohangla

Nyimbo za Ohangla huhusishwa na jamii ya Luo katika nchi ya Kenya. Inaaminika kuwa jina "Ohangla" huenda liliibuka katika mwaka wa 1940 kutokana na mtindo wa densi uliokuwa wa kasi ila ulikosa heshima kwa kuwa ulihusisha kauli za kingono kwenye maudhui na miondoko yake. Kutokana na mtindo huo wa densi, wazee wa jamii hii waliita *'miel ma ohangore'* (miondoko ya ajabu).

Hata hivyo, kulingana na Okong'o (2011) ngoma ya *Ohangla* ilichezwa miongoni mwa jamii ya Alego wakati wa sherehe za harusi. Okong'o anaeleza kuwa wakati wa densi, bwana harusi angetangaza kuwa bibi harusi 'alijitunza' kabla ya ndoa. Bwana harusi angesema '*an mane ahange'* (Mimi ndiye nilimvunja ubikira). Okong'o anaamini kuwa jina 'Ohangla' lilitokana na kauli hii.

Kulingana na Omolo-Ongati (2005), *Ohangla* katika jamii ya Waluo ilihusisha wimbo na uchezeshaji wa viungo vya mwili. Kulingana naye, *Ohangla* hujumuisha ngoma, kinanda, *orutu*, miongoni mwa vifaa vingine vya kitamaduni. *Ohangla* ilichezwa katika jamii ya Waluo mara nyingi nyakati za sherehe.

Kinyume na ilivyokuwa hapo awali ambapo *Ohangla* ilikuwa na dhima maalum katika jamii ya Waluo, utunzi wa *Ohangla* umebadilisha mtindo na dhima yake katika miaka ya hivi karibuni. Kabla ya mabadiliko haya, *Ohangla* ilikuwa na jukumu la kuendeleza mila za jamii husika. Jukumu hili

limeathiriwa na kuvumbuliwa kwa teknolojia na mahitaji ya kiuchumi ya binadamu.

Kulingana na Omondi (1992), katika jamii ya sasa, *Ohangla* huchezwa katika miktadha tofauti na kufurahiwa na hadhira yenye mila na desturi tofauti. Kulingana naye, nyimbo za *Ohangla* kwa sasa zinachezwa ili kutimiza mahitaji ibuka ya jamii. Kwa sasa, teknolojia imedhibiti *Ohangla* kiasi cha kuitoa nje ya mipaka ya kimila ya jamii ya Waluo.

Kuna watafiti kadhaa waliochunguza matumizi ya *Ohangla* katika jamii ya Luo. Nyakiti (2011) alichunguza majukumu ya nyimbo za kitamaduni zinazotokana na matumizi ya kinanda miongoni mwa baadhi ya wanamuziki kutoka jamii ya Luo. Omolo-Ongati (2005) naye alitafiti mtindo mseto unaodhihirika katika utendaji wa nyimbo za *Ohangla*. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa *Ohangla* hujumuisha ngoma, kinanda, *orutu*, miongoni mwa vifaa vingine vya kitamaduni.

Akumu (2012) alichunguza majukumu ya nyimbo za *Ohangla* katika sherehe mbalimbali kama vile mazishi na harusi. Naye Ochieng (2022) alichunguza asili na kua kwa muziki wa *Ohangla* miongoni mwa jamii ya Luo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa muziki wa *Ohangla* umekua na sasa unachezwa ili kutumbuiza watu na katika sherehe za mazishi na harusi. Ochieng anaeleza kuwa *Ohangla* haitumiwi tena katika kupitisha mila na tamaduni za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

3.2 Yaliyoandikwa kuhusu ubadilishaji msimbo

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu suala la ubadilishaji msimbo. Parkin (1974) alifanya utafiti kuhusu ubadilishaji msimbo kati ya watu wanaoishi katika mtaa wa Kaloleni, Nairobi. Alibainisha kuwa watu hubadili msimbo kwa mfano, kutoka Kiingereza, Kiswahili na lugha za kwanza kwa sababu ya ukabila na utabaka wa wahusika. Alibainisha kuwa lugha ya Kiingereza ilitumiwa sana na watu wa tabaka la juu na wanaotumia lugha za kwanza waliegemea katika ukabila.

Muthwii (1986) alichunguza matumizi ya lugha katika jamii ya wingi-lugha na umuhimu wa ubadilishaji msimbo. Mtafiti huyu alishughulikia lugha za Kiingereza, Kiswahili na Kalenjin. Utafiti huu ulitumia nadharia ya Uamilifu ya Gumperz (1982).

Muthuuri (2000) alichunguza ubadilishaji msimbo miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. Aliangazia mandhari ya uwingi lugha hasa wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Kikuyu. Alibainisha vijana hubadili msimbo wakiwa na nia ya kufanana au kutofautiana na wenzao. Utafiti huu ni tofauti na utafiti huu kinadharia na kimalengo.

Ogechi (2002) alichanganua ubadilishaji msimbo katika mazingira ya utatu lugha ambayo ulijumuisha Kiswahili, Sheng na Ekegusii. Kulingana na utafiti huu lugha za Kiingereza na Kiswahili zilichukuwa nafasi ya lugha solo. Utafiti huu ulibaini kuwa ubadilishaji msimbo ulichangiwa pakubwa na mfumo wa elimu na sera za lugha nchini Kenya. Kwa kuwa sera hizo zinapelekea Kiswahili na Kiingereza kuwa lugha zenye hadhi ya juu, wanajamii hutaka kupanda kitabaka haswa katika matumizi ya lugha.

Nthiga (2003) alifanya utafiti kuhusu mitindo na dhima za kubadili msimbo katika shule za chekechea. Utafiti huu ulionyesha kuwa watoto hubadili msimbo ili waweze kuwasiliana kwa urahisi na kwa njia inayoeleweka.

Mathooko (2004) alitafiti kuhusu mtagusano wa misimbo ipatikanayo katika mpaka wa Tharaka na Kamba ambapo Kitharaka na Kikamba huzungumzwa. Utafiti huu ulichunguza muundo wa jamii, uamilifu, ukawaida na utofauti wa lugha hizo. Utafiti huu ulipata kuwa usawa wa kileksia na kifonolojia ulisababisha mfanano katika mazungumzo baina ya lugha hizo. Utafiti ulibaini kuwa sababu za kisaikolojia na kisosholojia zilipelekea wazungumzaji kutumia lugha za majirani yao ili kutimiza malengo ya kijamii, haja ya kutaka kueleweka, kutambulika, kupendwa na pia kwa sababu ya kufanana kwa lugha hizo. Utafiti huu unatofautiana na utafiti huu kimalengo na kinadharia.

Munuku (2005) alifanya uchunguzi wa kubadili msimbo katika nyimbo za kisasa za *rap*. Aliangazia mitindo na mikakati ya ubadilishaji msimbo katika nyimbo za *rap* nchini Kenya na jinsi ambavyo hawa waimbaji hubadili msimbo ndani ya sentensi au katika vifungu vya maneno.

Wanjogu (2010) alifanya utafiti kuhusu athari na sababu za kubadili msimbo katika shule ya upili ya Akiba jijini Nairobi. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya Maridhiano ya mawasiliano iliyoasisiwa na Giles (1973) na kuthibitisha kuwa katika miktadha mingine, ubadilishaji msimbo ulitokana na hali ya kiutambuzi iliyotokana na jamii au sababu za kibinafsi.

Kimaiyo (2014) alichunguza vichocheo na majukumu ya ubadilishaji msimbo katika baadhi ya nyimbo za Kipsigis. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa wasanii wa Kipsigis hubadilisha ili kuziba pengo la kileksia, kuchekesha au kupunguza ukali wa maneno.

Utafiti huu ulijikita katika muktadha wa Kipsigis.

Ali, Malik na Jillan (2016) walitafiti kuhusu sababu za kuchanganya msimbo katika nyimbo za filamu za Kihindi. Kulingana nao, uchanganyaji msimbo katika filamu hutokana na ukweli kuwa uchanganyaji hufanya wimbo ukumbukike, huleta uwiano wa vina, na hutokana na matakwa ya watengenezaji filamu. Pia, uchanganyaji huo hutokana na kuona fahari, kupata umaarufu wa haraka, na kuonyesha usasa

Mabonga (2023) alichunguza kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya moduli ya masafa ya mulembe na moduli ya masafa ya sulwe. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya Maki iliyoasisiswa na Myers –Scotton (1993). Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa ubadilishaji wa msimbo huchochewa na sababu mbalimbali kama vile kufidia upungufu wa msamiati na kujitambulisha na kundi fulani.

Ingawa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu kubadili msimbo, ni dhahiri kuwa hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu aina za ubadilishaji msimbo katika nyimbo za *Ohangla*.

4.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Maki iliyoasisiwa na Carol Myers-Scotton (1993). Nadharia hii ilitumiwa kutokana na uwezo wake wa kutathmini aina za ubadilishaji msimbo hususan katika nyimbo. Nadharia hii inadai kuwa wazungumzaji huchagua lugha kuashiria seti za haki na wajibu, yaani, misimbo ya kijamii ya kidhahania inayotumiwa na wazungumzaji katika mtagusano wao.

Myers-Scotton (1913) alitumia nadharia hii kuelezea dhana ya muundo wa sarufi katika ubadilishaji msimbo na kisha baadaye kutumia dhana hiyo ya Maki kuelezea vichocheo vya ubadilishaji msimbo. Kulingana na naye nadharia hii hupendekeza kuwa wazungumzaji wanaelewa alama kuhusu misimbo ya kiisimu inayotumika katika maingiliano yoyote, ingawa uteuzi wa misimbo hutegemea mhusika na uhusiano na wengine. Katika nadharia hii, uteuzi wa msimbo hufanywa kimaksudi kwa kuwa unalenga kutimiza malengo fulani ya mawasiliano. Wazungumzaji hufanya uteuzi huu wakiwatarajia wasikilizaji wao kubainisha nia iliyopo kwenye msimbo fulani.

Kulingana na Myers-Scotton, msimbo unaweza kuwa na Maki au usiwe na Maki. Hali hii ndiyo msingi wa kuelezea vichocheo vya kisaikolojia na kisosholojia katika kuchagua msimbo mmoja au mwingine. Msimbo huweza kuwa wenye Maki au usio na Maki kwa kuzingatia matumizi yake katika jamii. Msimbo wenye Maki ni msimbo ambao hautarajiwi katika desturi za jamii ilhali msimbo usio na Maki hurejelea desturi na mila za jamii na kile kinachotarajiwa au kuonekana kuwa ni kawaida. Mzungumzaji hutambua aina ya msimbo utakaotumika kimakusudi. Msimbo usio na Maki huchukuliwa kuwa wa kawaida kwa sababu haubebi maana ya ziada kutokana na kubadilika kwake muktadha ukibadilika.

Kulingana na Lawrence (1999) mpangilio wa hali zinazopelekea kuwepo kwa hali fulani unapobadilika katika mazungumzo, hupelekea kuwepo kwa msimbo usio na Maki. Kwa mfano, watu wawili wanapokutana kwa mara ya kwanza watatumia msimbo ambao wote wanaulewa vizuri. Hata hivyo, wakigundua kuwa wanatoka katika eneo moja na jamii moja, wataanza kuzungumza kwa lugha yao asilia.

Kulingana na Myers-Scotton, msimbo wenye Maki hubeba maana ya ziada ya kijamii, na mzungumzaji anapotumia msimbo huu, ujumbe huwa na maana zaidi ya ile ya msingi na pia hueleza kusudi na mabadiliko katika kutangamana. Mzungumzaji anapotia Maki huzingatia uhusiano uliopo na tabia za mtu na hujua matokeo ya kuwepo kwa Maki katika msimbo.

Kulingana na Fernandez (2010), msimbo wenye Maki unaweza kuwa neno moja tu katika sentensi ambalo ni la lugha tofauti. Rose (2006) anaeleza kuwa anayetumia msimbo wenye Maki anachukuliwa kuwa kama mwanabiashara anayelenga kupata faida bila kuzingatia hatari au gharama. Nia yake kuu huwa kuonyesha ubunifu wake ambao hufananishwa na kamari; yaani uwasilishaji wake huwa wa bahati nasibu. Hivyo, muundo wake huweza kuonekana kwa kurudiwa, kusikika zaidi au kutiliwa mkazo.

Myers- Scotton aliingiza dhana ya lugha solo katika kuendeleza nadharia hii. Lugha solo ni lugha inayobeba muundo wa semi au inayojitokeza kwa wingi katika usemi. Hii ina maanisha kuwa katika ubadilishaji msimbo lugha moja huwa na uzito fulani na hujitokeza sana ikilinganishwa na nyingine. Lugha solo inaeleweka na hutumika kwa wingi. Lugha solo ni msingi mojawapo wa kupimia mtagusano wa lugha kwa sababu ni lugha inayotumika sana katika usemi. Upimaji huo umejikita katika asilimia ya lugha solo na jumla ya maneno kutoka kwa lugha nyingine.

Haki na majukumu ni kati ya vipengele muhimu katika nadharia hii ambavyo humwezesha mtu kupima umaki katika msimbo. Kipengele hiki huangazia dhana katika mazingira ambazo hupelekea kuwepo na mielekeo na matarajio ya wazungumzaji kuhusu mmoja wao kwa misingi ya matumizi ya lugha (Myers-Scotton, 1993). Rose (2006) anaeleza kuwa haki na majukumu hubaini mwingiliano wa matukio kutoka kwa jamii kwa

kuelezea tabia na vigezo muhimu katika jamii. Baadhi ya vigezo hivyo ni kama vile; jinsia, elimu, tabaka na kabila ambazo huwa kiwakilishi na kitambulisho cha washiriki.

Mihimili ya Nadharia ya Maki

i. Msimbo usio na Maki: Msimbo unaojitokeza hapa huwa ule unaojulikana na hivyo haubebi maana zaidi, hivyo lugha msingi ya Dholuo ilichukuliwa kuwa lugha isiyo na maki.
ii. Msimbo wenye Maki: Msimbo huu hubeba maana ya ziada ya kijamii na hivyo kuwa bora katika kueleza msimbo katika muktadha zaidi na ule wa kijamii.
iii. Seti za Haki na Majukumu: Hutengeneza mazingira ya msimbo kutumika na utarajio baina ya wazungumzaji.

5.0 Mbinu za utafiti

Utafiti ulikuwa wa kistahilifu na ulihusisha utafiti wa mtandaoni na maktabani. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2005) utafiti wa kistahilifu unahusu uchanganuzi wa vitu katika hali zao asilia na kujaribu kufasiri maana ambayo wanajamii huvipa vitu hivyo. Kothari (2004) anaeleza kuwa utafiti wa kistahilifu unahusisha mbinu zisizozalisha data za nambari. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo kwa kuwa mtafiti alilenga kuchanganua vitu katika hali zao asilia na kutoa maelezo kuvihusu. Muundo wa kimaelezo ulitumiwa na mtafiti kuchanganua matini katika nyimbo za *Ohangla* katika jamii ya Waluo.

Mtafiti alitumia sampuli kusudio ili kuteua nyimbo nne za Ohangla zilizochanganuliwa kama sampuli ya utafiti. Mtafiti aliteua nyimbo mbili za Prince Indah na mbili za Vicky B. Matata. Nyimbo hizi ziliteuliwa kwa sababu zilidhihirisha visa vya ubadilishaji mwingi wa msimbo. Mtafiti alitumia *wi-fi*, simu na tarakilishi katika kukusanya data. Mtafiti alitumia simu na tarakilishi kuingia kwenye mtandao wa *Youtube* ili kupata na kupakua nyimbo za *Ohangla* zilizochanganuliwa.

Data ya utafiti ilikusanywa kwa kupakua na kusikiliza nyimbo za *Ohangla* zilizoteuliwa kama sampuli ya utafiti kisha kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya utafiti, kuirekodi. Utafiti ulitumia unukuzi kamili kurekodi data ya utafiti. Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumiwa na mtafiti kwa sababu utafiti huu ulilenga kuchunguza sifa ya lugha katika nyimbo za *Ohangla* ili kuipa maana katika muktadha husika. Enon (1998) anasema kwamba huu ni uchanganuzi unaomhitaji mtafiti kuzitolea data zake maelezo.

Mtafiti pia alitumia tafsiri huru kutafsiri data ya utafiti kutoka kwa lugha solo (*Dholuo*) hadi lugha ya utafiti ambayo ni Kiswahili. Tafsiri huru ilitumiwa ili kuhifadhi maana asilia ya matini katika wimbo. Isitoshe, lugha ya *Dholuo* ilichukuliwa kuwa msimbo usio na maki huku Kiswahili na Kiingereza zikichukuliwa kuwa msimbo wenye maki.

6.0 Aina za ubadilishaji msimbo katika baadhi ya nyimbo za Ohangla

Makala hii ililenga kuchunguza aina za ubadilishaji msimbo katika baadhi ya nyimbo za Ohangla. Fasili mbalimbali zimetolewa na wataalam anuwai kuhusu dhana ya kubadili msimbo kama ilivyodokezwa hapo awali. Hata hivyo, makala hii ilitumia maelezo ya Myers-Scotton kuhusu dhana ya ubadilishaji msimbo. Kulingana naye, kubadili msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo, bila kutohoa fonolojia ya lugha moja ili iingiliane na nyingine. Alitumia dhana ya kubadili msimbo kujumuisha dhana za kuchanganya na kuhamisha msimbo. Utafiti huu unakubaliana na Kachru (1978) kuwa kuchanganya na kuhamisha lugha ni mbinu zinazotumiwa kubadili lugha.

Kulingana na Myers-Scotton kuna aina tatu za kubadili msimbo, yaani, kubadili msimbo ndani ya sentensi, kubadili msimbo baina ya sentensi na kubadili msimbo kileksia. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa aina zote tatu za ubadilishajij msimbo hutumiwa katika nyimbo za *Ohangla*. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa ubadilishaji wa msimbo ndani ya sentensi hutumiwa kwa asilimia kubwa kuliko aina zingine.

Utafiti huu pia umebaini kuwa watunzi wa nyimbo za *Ohangla* hutumia mikondo miwili ya ubadilishaji msimbo, yaani, ubadilishaji msimbo kutoka msimbo usio na maki hadi msimbo wenye maki na ubadilishaji msimbo kutoka msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki. Utafiti huu ulichukua lugha ya *Dholuo* kama lugha solo hivyo kuwa msimbo usio na maki. Makala hii ilichanganua aina zifuatazo za ubadilishaji msimbo:

6.1 Ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi

Kulingana na Hoffman (1991) ubadilishaji msimbo wa aina hii hutokea ndani ya sentensi au mipakani mwa sentensi.

Mifano A:

1. *Gima mora en* **sura** *mari*

Tafsiri: Kinachonifurahisha ni sura yako

2. *Ni* **pamba** *goli maondisi*

Tafsiri: Ati pamba (nguo) inakutoa vizuri

3. Mano e **nia** *gi* **toto** *kethoni*
Tafsiri: Hiyo ndiyo nia yao toto ya kukuharibia
4. Wanager **ghorofa** *moro*
Tafsiri: Tutajenga ghorofa jingine
Chanzo- *Nyanango- Vicky B Matata*

Katika mifano A, mtunzi wa wimbo huu alianza wimbo wake kwa msimbo usio na maki ambao ni *Dholuo* kisha akashirikisha msimbo wenye maki ambao ni Kiswahili. Katika muktadha huu vipashio vya Kiswahili vimechopekwa ndani ya lugha solo ambayo ni *Dholuo*. Katika mfano 1 na 4, msanii huyu ametumia maneno 'sura' na 'ghorofa' ambayo ni maneno ya Kiswahili ili kufidia ukosefu wa misamiati inayoweza kutumiwa kurejelea maneno haya katika lugha msingi ambayo ni *Dholuo*. Mifano 2 na 3 inaonyesha umuhimu wa kuongeza ladha katika wimbo kwa kutumia maneno yanayoibua hisia za mapenzi.

Mifano B:

5. Ng'ami hero donge ihero makata tweu e **jela** *pile to pod ihere ahera* mama
Tafsiri: Unayempenda si unampenda hata kama kila siku inawafunga kwenye jela bado unampenda tu mama

6. Ling'aling'a ah **rembo**
Tafsiri: Nyamaza tu mrembo

7. Ine **charger** *machajo hera* mama *ooh*
Tafsiri: Wewe ndiwe chaja inayoongeza mapenzi mama
Chanzo: *Mimi na Wewe- Prince Indah*

Katika mifano B, mtunzi kwa kukosa misamiati misingi katika msimbo usio na maki, ametumia maneno 'jela' na 'charger' ili kufidia upungufu huo wa misamiati. Vilevile, lugha ya *Dholuo* haina misamiati inayoweza kutumiwa kurejelea vifaa vya kiteknolojia kama vile 'charger'. Hata hivyo, mtunzi ametumia neno 'rembo' kudhihirisha anavyohisi kwa mrejelewa katika wimbo husika.

Mifano C:

8. Indah ma wuo nyandare **sauti yangu**
Tafsiri: Indah mwana wa nyandare sauti yangu

9. Iluonga **chocolate** *aluongi* **lollipop**
Tafsiri: Unaniita chocolate nami nakuita lollipop

10. Hera nochako **pole pole**
Tafsiri: Mapenzi yalianza pole pole

11. Jaber **kwa bahati mbaya** mama *onge*
Tafsiri: Mrembo kwa bahati mbaya mama hayuko

12. Mummy *kibedo buta* **wasiwasi** *onge*
Tafsiri: Mummy ukikaa karibu nami wasiwasi hakuna

13. Mama meth a metha **pesa** *nitie*
Tafsiri: Mama kunywa tu pesa zipo

14. Kwa bahati mbaya baba *onge*
Tafsiri: Kwa bahati mbaya baba hayuko
Chanzo: *Nyar Joluo- Prince Indah*

Katika mifano C, mbali na kupachika misamiati mbalimbali, mtunzi wa wimbo huu pia ametumia virai vya Kiswahili ili kubadilisha msimbo. Mfano wa 8, 'sauti yangu' ambacho ni kirai, unaonyesha ubadilishaji msimbo uliolenga kudhihirisha mtunzi aliye na umilisi wa msimbo wa zaidi ya mmoja. Misamiati 'chocolate'na 'lollipop' katika mfano wa 9 inadhihirisha ubadilishaji msimbo uliotekelezwa ili kufidia upungufu wa misimati inayoweza kutumiwa kurejelea dhana hizi katika msimbo usio na maki.

Hata hivyo, kutokana na mazoea ya kutumia misamiati hii katika lugha solo, katika mfano wa 10, wa 12 na wa 13, mtunzi amebadilisha msimbo kwa kutumia maneno 'pole pole', 'wasiwasi' na 'pesa' mtawalia. Misamiati hii inapatikana katika msimbo usio na maki. Katika mfano wa 11, mtunzi ametumia msimbo wenye maki 'kwa bahati mbaya' ambao ni kirai, kuonyesha hisia zake kwa hadhira, hisia za kumpoteza mamake. Mfano wa 14 unaonyesha ubadilishaji msimbo ulioanza kwa msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki. Katika muktadha huu, msimbo wenye maki ni Kiswahili huku usio na maki ukiwa Dholuo.

Mifano D:

15. Lando oberana **nitakupenda** *forever*
Tafsiri: Mrembo wangu nitakupenda milele
16. Ine chwechna beb **chaguo la moyo** *tek pingo*.
Tafsiri: Wewe ndiwe mpenzi wangu, chaguo la moyo ni vigumu kulipinga

17. Aah! *Omit* **sana** *kiwacho adierii*
Tafsiri: Aah! Ni matamu sana ukweli ukisemwa

18. Yanayojiri nimepata love *mowilo wiya*
Tafsiri: Yanayojiri nimepata mpenzi ambayo yamenikanganya

19. Ukicheza *to ogwari*
Tafsiri: Ukicheza inakukwaruza

Chanzo: Ma to Mara- Vicky B Matata

Katika Mifano D, Mfano wa 15 unaonyesha ubadilishaji msimbo ambao mtunzi ametumia kusisitizia mapenzi yake kwa mrejelewa. Katika mfano huu, mtunzi ameshirikisha lugha ya Kiingereza ili kusisitiza hisia zake kwa anayechukuliwa kuwa mpenzi wake. Ubadilishaji msimbo katika mfano wa 16 unadhihirisha hisia za mapenzi za mtunzi kwa mrejelewa. Katika mfano wa 17, mtunzi ametumia msimbo wenye maki 'sana' kutokana na mazoea ya kutumia neno hili katika lugha solo. Mfano wa 18 na wa 19 unaonyesha ubadilishaji msimbo ambapo msanii ameanzisha mistari yake ya wimbo kwa lugha bebwa ambayo ni Kiswahili kisha kumaliza na lugha solo ambayo ni *Dholuo*.

6.2 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi

Hoffman (1991) anaeleza kuwa aina hii ya ubadilishaji msimbo hutokea katika usemi wenye sentensi kutoka lugha mbili tofauti. Ubadilishaji huu ndio huchukuliwa kama kuhamisha msimbo. Katika muktadha huu wa utafiti, mistari iliyochanganuliwa ilianza kwa sentensi iliyotungwa kwa msimbo usio na maki (*Dholuo*) kisha kutamatika kwa sentensi iliyotungwa kwa msimbo wenye maki (Kiswahili/Kiingereza).

Mifano E:

20. Hera manyo kende mama eeh x2
Hera manyo mare mama eeh eeh, Lelilee ooh
Najipa kwako toka kwa mtimaa x2
Kwajili yako mimi naimba x2
Mimi na wewee eeh (mimi nawewehh) x4
Chanzo: *Mimi na Wewe- Prince Indah*

Katika mfano E, msanii amebadilisha msimbo baada ya kuacha lugha solo ya *Dholuo* ambayo ndiyo lugha msingi ya utunzi kisha kutunga sehemu hii ya muziki kwa msimbo wenye maki ambao ni Kiswahili. Ubadilishaji wa msimbo katika muktadha huu ulifanyika kwa lengo la kusisitiza ujumbe kwa hadhira.

6.3 Ubadilishaji msimbo wa Kileksia

Huu ni ubadilishaji msimbo unaotokea katika neno kwa kupachika mofu ambishi za lugha solo katika maneno ya lugha bebwa katika mazingira ya sentensi. Kulingana na Hoffman (1991) aina hii ya ubadilishaji msimbo hutokea katika neno. Myers-Scotton (1993) anaeleza kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea katika neno ili kutimiza majukumu mbalimbali kama vile kufidia upungufu wa msamiati au kujinasibisha na kundi fulani.

Mfano F:
21. *Jogo gombo* ***maionjo aonja***
Tafsiri: Watu hao wanatamani wa kuonjwa tu.
22. ***Mavuka*** *kumoro mabor ahinya*
Tafsiri: Ya kunivusha sehemu mbali sana
Chanzo: Nyanango- Vicky B Matata

Katika Mfano F, ubadilishaji msimbo wa kileksia umejitokeza katika maneno 'maionjo', 'aonja' na 'mavuka'. Katika maneno 'maionjo'na 'mavuka', msanii amebadilisha msimbo kwa kupachika mofimu 'mai' na 'ma' katika leksia za Kiswahili 'onja' na 'vuka' mtawalia. Katika msimbo usio na maki, mofimu hizi hutumiwa kurejelea kifaa kinachotekelezwa. Hivyo, katika muktadha huu mofimu hizi hurejelea 'anayeonjwa' na 'kinachovukisha' mtawalia. Leksimu 'a' katika leksia 'aonja'imetumiwa kudokeza uwezekano wa kufanyika kwa kitendo husika. Ubadilishaji msimbo katika mfano wa 21 umetokea kutokana na mazoea ya kutumia leksia 'onja' katika lugha solo. Katika mfano wa 22, ubadilishaji wa msimbo umetokea ili kiziba pengo la kileksia katika lugha solo kama inavyojitokeza katika Mifano G.

Mifano G:

23. *Ine charger na* ***machajo*** *hera mama ooh*
Tafsiri: Wewe ndiwe chaja yangu inayoongeza mapenzi mama

24. *Kata* ***kakoso*** *tich mama wadag gi kwee e odwa*
Tafsiri: Hata nikikosa kazi tuishi kwa amani kwetu.
Chanzo: *Mimi na Wewe- Prince Indah*

Mfano wa 23 katika Mifano H pia unaonyesha matumizi ya mofu 'ma' ya kitumizi katika neno 'chaja'. Leksimu hii hutumiwa kama kiwakilishi cha mtendaji/kitendaji katika lugha solo ambayo ni *Dholuo*. Ubadilishaji huu wa msimbo umetokea ili kufidia upungufu wa msamiati wa kurejelea hali ya 'kuchaji'. Katika mfano wa 24, mtunzi kutokana na mazoea ya kutumia neno 'kosa' katika lugha solo, amebadilisha msimbo kileksia kwa kupachika mofimu ya masharti ya nafsi 'ka' katika leksia 'kosa'.

Mifano H:

25. *Ah! WhatsApp nikanyo ne* ***wachat*** *kodi mum*
Tafsiri: Ah! Katika *WhatsApp* yako tulichati mum.
Chanzo: *Nyar Joluo- Prince Indah*

Katika mfano huu, msanii amebadilisha msimbo kwa kupachika leksimu 'wa' katika neno *chat*. Katika muktadha huu, leksimu 'wa' katika msimbo usio na maki hudokeza wahusika katika nafsi ya kwanza wingi. Kwa kuwa leksia 'chat' ni

geni katika msimbo usio na maki, ubadilishaji msimbo umefanywa ili kufidia pengo la kileksia.

7.0 Hitimisho

Makala hii imechanganua aina za ubadilishaji msimbo katika baadhi ya nyimbo za Ohangla. Utafiti umebaini kuwa wasanii wa nyimbo za *Ohangla* hutumia aina tatu za ubadilishaji msimbo; yaani, ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi, ubadilishaji msimbo baina ya sentensi na ubadilishaji msimbo kileksia. Pia, utafiti umebaini kuwa katika kubadilisha msimbo, wasanii wa nyimbo za *Ohangla* hutumia mikondo miwili ya ubadilishaji msimbo, yaani, ubadilishaji msimbo unaonza kwa msimbo usio na maki hadi msimbo wenye maki na ubadilishaji msimbo unaonza kwa msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki. Utafiti pia umegundua kuwa ubadilishaji msimbo hutekelezwa ili kutimiza majukumu fulani katika wimbo kama vile kufidia upungufu wa msamiati au kusisitiza jambo fulani.

Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kubadili msimbo katika muktadha wa Ohangla ni jambo la kawaida linalotekelezwa na wasanii wa nyimbo hizi aidha kwa kufahamu au bila kufahamu, ingawa kuwepo kwa hali hii hutekeleza majukumu fulani ya kiisimu katika nyimbo hizi. Kwa kuwa utafiti huu ulijikita tu katika kuchunguza aina za ubadilishaji msimbo katika nyimbo za Ohangla, utafiti anapendekeza umma ihamisishwe kuhusu ubadilishaji msimbo katika nyimbo hizi ili kuwanufaisha hadhira.

Marejeleo

Akinseye, T. A. (2016). 'Exploring radical bilingualism switches in selected Osundare's Poetic Idiostyle' in language and style in *Niyi Osundare's Poetry Selection from Osundare Research Conference TASUED, 2016 Edt by Ogunsuji Ayo, and Yomi Okunowo Ijagun*: TASUED Press

Akumu, J. (2012). *A Musical Analysis of Selected Luo Ohangla Songs*. Unpublished MA Thesis, Maseno University.

Ali, M., Malik, N. & Jillan, S. (2016). 'A critical analysis of intra sentential code mixing in Indian film songs.' *Special issue, Vol. 28, pp. 2019-2027.*

Arifin, Z. (2018). *Language use in multilingual societies*. London: Interlingual Press.

Bokamba, G. (1989). "Are there Syntactic constraints on code-mixing." *World Englishes 8.3 (1989): 277-292.*

Enon, C. (1998). *Education research and measurement*. Kampala

Fernandez, J. (2010). *A structural and functional analysis of codeswitching in Mi Vida Gitana `My Gypsy Life,' a bilingual play"*. MA Thesis: Portland State University

Giles, H. (1973). Accent mobility: A model and some data. *Anthropological Linguistics, 15(2), 87-105*

Gumperz, J. (1982). *Discourse strategies*. Cambridge: Cambridge University Presss.

Hoffman, C. (1991). *An Introduction to Bilingualism*. New York: Longman.

Kachru, B. (1978). "*Code- switching as a communicative strategy in India". SavilleTroike, Muvie (wah). Linguistics and Anthropology.* Washington: Georgetown University

Kimaiyo, P. (2014). *The markedness model approach to the motivation and functions of code-switching and code-mixing: A case study of selected Kipsigis songs*. (Unpublished M.A Thesis) University of Nairobi.

Kothari, C. (2004). *Research methodology: Methods and techniques (2nd Ed.)*. New Delhi: New Age International Publishers.

Lawrence, D. (1999). Code switching angels in Afrikaans: An instrument of effective communication. *Journal of Language Teaching 33, 265-274.*

Mabonga, I. (2023). *Tathmini ya kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya moduli ya masafa ya Mulembe na moduli ya masafa ya SULWE*. (Unpublished M.A Thesis) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mathooko, P. (2004). *Towards an intergrative perspective of linguistic accommodation: A case study of Kikamba and Kitharaka*. (Unpublished Phd Thesis) Kenyatta University.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (2005). *Research methods: Quantitative approaches*. Nairobi: ACTS Press.

Munuku, A. (2005). Code switching in the contemporary Kiswahili rap song. (Unpublished Masters Thesis) Kenyatta University.

Muthuuri, D. (2000). *Code switching among Kenyatta University multilingual community.*, Kenyatta University.

Muthwii, M. J. (1986). *Language use in plurilingual societies. The significance of code-switching*

English/Kalenjin. (Unpublished M.A Thesis) University of East Anglia.

Myers-Scotton, C. (1993). *Social motivations for code-switching-Evidence from Africa*. Oxford: Clarendon Press.

Nthiga, P.M. (2003). *Patterns and functions of code switching in pre- primary classroom discourse in selected schools at Kasarani Division, Nairobi*. (Unpublished M.A Thesis) Kenyatta University.

Nyakiti, C. (2011). Onanda: A Contemporary Luo Musical Genre. *International Council for Traditional Music (ICTM) 41st World Conference*. St. John's, Newfoundland, Canada.

Ochieng, V. F. (2022). *Origins and evolution of Luo people's folklore music: The case of Ohangla genre in Siaya County, Kenya*. University of Nairobi.

Ogechi, N. (2002). *Trilingual code switching in Kenya-Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng* (Published Doctoral dissertation) University of Hamburg

Okong'o, J. (2011). Ohangla music as a parodic genre and postcolonial Luo experience. *Africa Today*, *57*(3), 24–38.

Omolo-Ongati, R. (2005). The concept of aesthetics as applied to and in the musical experience of the Luo: Maseno. *Journal of Education Arts and Science, S(1), 31-42*.

Omondi, W. (1992). *Problems in the Study of Ethnomusicology in Kenya*. Nairobi: University of Nairobi.

Parkin, D. (1974*). Language switching in Nairobi*. Nairobi: Oxford University Press

Rose, S. (2006). *The functions of code-switching in a multicultural high school*. Mphil thesis in Intercultural Communication: (Published Masters Thesis) Stellenbosch University.

Wahyuni, D. (2017). *An analysis of code switching and code mixing used in song lyrics soundtrack. Album of Goblin Korean Drama (143211012)*. (Published Undergraduate thesis) State Islamic Institute of Surakarta.

Wanjiru, M. (2014). *Code-mixing and code-switching in contemporary Kenyan music* Unpublished Master's Thesis, Kenyatta University.

Wanjogu, V. (2010). *Sababu na athari za ubadilishaji msimbo shuleni katika Shule ya Upili ya Akiba*. (Unpublished Masters Thesis) Chuo Kikuu cha Nairobi.